Viongozi Vipofu Wa Vipofu

(Blind Leaders of the Blind)

Na

Ellis P. Forsman

Viongozi Vipofu Wa Vipofu

(Blind Leaders of the Blind)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 05, 2011

Viongozi Vipofu Wa Vipofu

Mat.15:12-14

Unaweza kumwamini nani kuhusiana na maswala ya kidini? Watu wengi wa kidini wa dunia hii wanawaamini wahubiri wao, kuhani, au shemasi. Wanaamini kwamba "mtu wa Mungu" anapaswa kuaminiwa.

Pia, Biblia haiongelei mara nyingi kuhusu viongozi wa dini.

Paulo alionya kuhusiana na "mbwa mwitu wakali" wasilihurumie kundi la Mungu. Mdo. 20:29-30, "*Najua mimi ya kuwa baada ya kuondoka kwangu mbwa mwitu wakali wataingia kwenu, wasilihurumie kundi; tena katika ninyi wenyewe watainuka wakisema mapotovu, wawavute hao wanafunzi wawaandamie wao.*"

Petro aliandika kuhusu "waalimu wa uongo" wakileta uharibifu wa kupotosha. 2 Pet. 2:1-2, "*Lakini kuliondokea manabii wa uongo katika wale watu, kama vile kwenu kutakavyokuwako waalinu wa uongo, watakaoingiza kwa werevu uzushi wa kupoteza, wakimkana hata Bwana aliyewanunua, wakijiletea uharibifu usiokawia. Na wengi watafuata ufisadi wao; na kwa hao njia ya kweli itatukanwa.*"

Watu kama hao wanaweza kutambua kuwa wanaangamiza watu wa Mungu. Siyo wote wanaoposhwa wanafanya hivyo kwa kujua.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake kuhusu "*viongozi vipofu wa vipofu*". Mat. 15:12-14, "*Ndipo wanafunzi wake walipomwendea, wakamwambia wajua ya kuwa Mafarisayo walipolisikia neno lile walichukizwa? Akajibu akasema kila pando asilolipanda Baba yaangu wa mbinguni litang'olewa. Waacheni hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimuongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.*"

Kuwa "*vipofu"* wenyewe hawawezi kutambua jinsi wanavyowaongoza wengine. Hata hivyo, matokeo ya mwisho bado yanafanana. Hao wanaoongozaa vibaya bado "*wanatumbukia shimoni*" na wanaangamizwa. Mat. 15:14, "*Waacheni hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.*" Isa. 9:16, "*Kwa maana wawaongozao watu hawa ndio wawakoseshao, na hao walioongozwa na watu hao wameangamia.*"

Iwe umeongozwa na "*mwalimu wa uongo*", au na "*kiongozi kipofu*", wote mmeangamizwa.

Kwamba sisi wenyewe kwa kutokuona tusimfuate kiongozi kipofu; tabia za kiongozi kipofu ni zipi? Tunawezaa kujihakikisha vipi kwamba hatuongozwi na kiongozi kipofu?

Haya ni maswali tunayofaa kujibu katika somo hili.

Petro akiwa na mengi ya kusema kuhusu waalimu wa uongo (2 Pet. 2), Yesu pia alikuwa na mengi zaidi ya kusema juu ya viongozi vipofu.

Tabia za kiongozi kipofu

Wanashikilia mafundisho ya wanadamu.

Hii ndio ilikuwa swala la mafarisayo katika Mat. 15. Wanapenda kuweka mafundisho yao juu kuliko neno la Mungu. Mat. 15:3, "*Akajibu akawaambia mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu?*" Mat. 15:6, "*…Asimheshimu baba yake na mama yake. Mkalitangua neno la Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu.*" Mat. 15:9, "*Nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*"

Viongozi vipofu leo watafanya hivyo hivyo:

- Wakifundisha mafundisho yao.
- Wasijue kwamba kile wanachofundisha kimetoka kwa wanadamu, siyo Mungu.

Wakifanya utofauti mahali ambapo Mungu hajaweka.

Hili lilikuwa ni tatizo la Mafarisayo katika Mat. 23, ambapo wanaitwa "*vipofu*" mara tano. Walitengeneza utofauti mzuri kati ya aina za nyapo ambazo mtu anapaswa kuapa. Mat. 23:16-22, "*Ole wenu viongozi vipofu ninyi msemao, mtu atakayeapa kwa hekalu si kitu; bali mtu atakayeaapa kwa dhahabu ya hekalu amejifunga. Wapumbavu ninyi ni vipofu; maana ni ipi iliyo kubwa, ile dhahabu, au lile hekalu liitakasalo dhahabu? Tena mtu atakayeapa kwa madhabahu si kitu, bali mtu atakayeapa kwa sadaka iliyo juu yake amejifunga. Vipofu ninyi maana ni ipi iliyo kubwa, ile sadaka au ile dhabahu iitakasayo sadaka? Basi yeye aapaye kwa madhabahu, huapa kwa hiyo, na kwa vitu vyote vilivyo juu yake. Naye aapaye kwa hekalu, huapa kwa hilo na kwa yeye akaaye ndani yaake. Naye aapaye kwa mbingu, huapa kwa kiti cha enzi chaa Mungu, na kwa yeye aketiye juu yake.*"

Viongozi vipofu watafanya hivyo mara nyingi hata leo, wakifanya tofauti mzuri ili kwamba mtu asilishike neno la Mungu; wakisema baadhi ya maagizo ya Mungu ni muhimu kwa wokovu, lakini zingine sio (ubatizo).

Kuacha maagizo ya Mungu bila kukamilika.

Tena, Mafarisayo walikosea katika hili, ambapo waliitwa "*viongozi vipofu*". Waliacha mambo "*mazito*" ya sheria ya Mungu pasipo kukamilika. Mat. 23:23-24, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jirani, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache. Viongozi vipofu wenye kuchuja mbu na kumeza ngamia.*"

Walisisitiza zaka, lakini wwakaachaa mambo makuu ya sheria, rehema, imani; hivyo wangechuja mbu, lakini wakameza ngamia.

Viongozi vipofu leo wanafanya hivyo, lakini wakirudi nyuma. Wanaharaka katika mambo "*mazito*" , na kuacha yale wanayochukulia kuwa ni "mepesi" bila kuyatimiza.

Lakini Yesu alisema tunapaswa kuyafanya yote, tusiache yo yote bila kukamilika!

Tukitazama tu katika utu wan je.

"*Mafarisayo vipofu*" walitazama tu kwa nje.

Mat. 23:25-28, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnasafisha nje ya kikombe na chano na ndani yake vimejaa unyang'anyi na kutokuwa na kiasi. Ewe Farisayo kipofu, safisha kwanza ndani ya kikombe, ili nje yake nayo ipate kuwa safi. Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mmefanana na makaburi yaliyopakwa chokaa, nayo kwa nje yaonekana kuwa mazuri, bali ndani yamejaa mifupa ya wafu, na uchafu wote. Vivyo hivyo ninyi nanyi, kwa nje mwaonekana naa watu kuwa wenye haki, bali ndani mmejaa unafiki na maasi.*"

Walikuwa wanajali sana kutunza mila na desturi za usafi, wakiwa tayari kulazimisha, kujipenda wenyewe, unafiki, na kutokuwa na sheria.

Leo viongozi vipofu wanafuraha kwa kutokea kwa mafanikio, kama kuwa na majengo makubwa, wafuasi wengi, na kuwakubali watu ambao hawajaitii injili kaatika huduma za kanisa.

Tabia zingine.

Kutoka katika kifungu hiki (Mat.23) ambapo Yesu anawakea Mafarisayo, tunaona baadhi ya tabia za hao viongozi vipofu. Tuweke katika ufupisho haraka:

- Mat. 23:1-4, "*Kisha Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, akassema, Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti*

cha Musa; basi yoyote watakayowaambia myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao msitende; maana haao hunenaa lakini hawatendi. Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao."

- Mat. 23:5, "*Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu; kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao.*"
- Mat. 23:6-7, "*Hupenda viti vya mbele katika karamu na kuketi mbele katika masinagogi, na kusalimiwa masokoni na kuitwa na watu Rabi.*"
- Mat. 23:8-10, "*Bali ninyi mssiitwe Rabi, maana mwalimu wenu ni mmoja, nanyi nyote ni ndugu. Wala msimwite mtu baba duniani; maana Baba yenu ni mmoja, aliye wa mbinguni. Wala msiitwe viongozi; maana kiongozi wenu ni mmoja naye ni Kristo.*"
- Mat. 23:13, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnawafungia watu ufalme wa mbinguni; ninyi wenyewe hamwingii, wala wanaoingia hamwaachi waingie.*"
- Mat. 23:14, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnakula nyumba za wajane, na kwa unafiki mnasali sala ndefu; kwa hiyo mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi.*"
- Mat. 23:15, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnazunguka katika baahari na nchi kavu ili kumfanya mtu mmoja kuwa mwongofu; na akiisha kufanyika mnamfanya kuwa mwana wa jehanam mara mbili zaidi kuliko ninyi wenyewe.*"
- Mat.23:29-31, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnayajenga makaburi ya manabii na kuyaapamba maziara yaa wenye haki, na kusemaa kama sisi tungalikuwako zamani za baba zetu, hatungalishirikiana nao katika damu ya manabii. Hivi mwajishuhudia wenyewe, ya kwamba ninyi ni wana wao waliowaua manabii.*"

Hii inakuwa kama walivyo viongozi wengi wa dini leo, hasa katika runinga kama hatuko makini, tunaweza kupotoshwa nao.

Hii inatupeleka katika kipengele chetu kingine…

Jinsi ya kutopotoshwa na “viongozi vipofu”

Wasikilize kwa makini.

Tunapaswa kuwa na tabia kama za Waberoya. Mdo. 17:11, “*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*”

Paulo alipoingia mjini, “*walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo*”. Hii inaonyesha jinsi walivyomsikiliza Paulo – wakisikiliza kwa makini mabo aliyokuwa anafundisha.

Tunapaswa kwanza kuwapa walimu wote usikivu mwema na umakini na tukitafuta kuelewa hakika yale wayasemayo. Inaitajika tuwe wasikivu wazuri.

Wengi wanapotoshwa kwa sababu hawajajifunza kusikiliza kwa makini kile wanachofundishwa! (Unasikiliza vizuri kiasi gani?).

Yachunguze maandiko kila siku.

Huu ulikuwa uungwana mzuri moja wapo ya Waberoya. Mdo. 17:11, “*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*”

Baada ya kusikiliza kwa makini, walienda nyumbani na kulinganisha kile alisema Paulo kuhusu maandiko. Hawakukubali kirahisi alichokisema Paulo.

Kwa bahati mbaya, wengi leo hawana elimu ya Biblia. Hawafuatilii Biblia zao mtu anapofundisha au kuhubiri. Hawasomi Biblia zao kila siku.

Kushindwa kufanya mambo haya inamuacha mtu katika hali ya upofu, wakishindwa kujua neno la Mungu ni niniau wengine hufundisha mapokeo ya wanadamu.

Hitimisho

Mwisho wa viongozi vipofu utakuwa nini, na wale wanao wafuata? Kama mimea, “watang’olewa” na Baba wa Mbinguni. Mat. 15:13, “*Akajibu akasema, kila pando asilolipanda Baba yangu wa mbinguni litang’olewa.*”

Wote wawili “watatumbukia shimoni”. Mat. 15:14, “*Waacheni hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili.*”

Hata kama we ni mtu wa dini, wanadhani kwamba wanamtumikia Bwana, lakini Yesu atawaambi: Mat. 7:21-23, “*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*”

Nani alaumiwe, kama watu wanapotoshwa na viongozi vipofu? Kiongozi kipofu atawajibika, lakini si jumla.

Kama watu ni vipofu, ni kwa sababu wamefunga macho yao wenyewe. Mat. 13:15, “*Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, wakaongoka nikawaponya.*”

Mfano wa Waberoya na itukumbushe kilicho chema tusije tukaongozwa na viongozi vipofu, na hivyo tuone na kusikia alichosema Yesu kuwa kwelikwetu sisi: Mat. 13:16-17, “*Lakini heri macho yenu kwa kuwa yanaona; na masikio yenu kwa kuwa yanasikia. Kwa maana amini nawaambia, manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi, wasiyasikie.*”